

**HOTUBA YA UFUNGUZI WA KIKAO CHA WADAU WANAOTOA  
HUDUMA MKOANI DAR ES SALAAM ILIYOTOLEWA NA  
KAIMU MKUU WA MKOA TAREHE 29 SEPTEMBER, 2008  
KWENYE UKUMBI WA KARIMJEE**

Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa.

Mkurugenzi wa Jiji.

Wakurugenzi wa Manispaa.

Viongozi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali.

Viongozi wa Madhehebu ya dini.

Wawakilishi wa Mashirika yasiyo ya kiserikali.

Wawakilishi wa Vyombo vya Habari.

Maafisa wa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri.

Mabibi na mabwana.

Awali ya yote, nashukuru kwa kunipa heshima kuja kuwafungulia Mkutano huu muhimu kwa maendeleo ya Mkoa. Ninyi ni wadau muhimu sana katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Hivyo kukutana pamoja na kuelezana kila mmoja anafanya nini kutasaidia sana kuboresha ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi wetu ambao ndiyo matarajio yao.

Kabla ya muundo mpya wa Tawala za Mikoa Tanzania Bara ulioanza kutekelezwa mwaka 1997, huko nyuma chini ya madaraka mikoani kulikuwa na kikao rasmi (Forum) kilichokuwa kikijulikana kama timu ya Menejimenti ya Mkoa (Regional Management Team – RMT) kikao hicho kilikuwa kikiwakutanisha wadau kujadili masuala ya maendeleo kabla ya kuwasilishwa kwenye kamati ya Maendeleo ya Mkoa (RDC). Waliweza kuchambua na kuelezana mambo mengi ya maendeleo.

Siku hizi kikao kama hicho hakipo kwa kuwa madaraka mengi zimepewa mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) ambazo ndizo zenye Kamati mbalimbali za kudumu pamoja na Baraza la Madiwani kupitia wawakilishi wa wananchi.

Kwa upande wa Serikali Kuu ngazi ya Mkoa kuna vikao vya Kamati ya Ushauri za Wilaya (DCC) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ambazo zinajadili taarifa za maendeleo na kutoa ushauri chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa (Regional Administration Act Na. 19 ya 1997). Pamoja na vikao hivyo rasmi kikao hiki cha kitaalamu ni muhimu kiwe kinafanyika kila inapobidi ili kujadili utoaji huduma kwa jamii na kubadilishana uzoefu utakaosaidia kuboresha zaidi huduma zetu.

Ndugu wadau, napenda kunukuu mgawanyo wa majukumu baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kama yalivyoainishwa kwenye Waraka wa utumishi Na. 1 wa mwaka 1998.

- Serikali Kuu katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera za Serikali na kuhakikisha kuwa watekelezaji mbalimbali wanazingatia maelekezo ya Serikali na kwamba malengo yaliyowekwa na Taifa yanafikiwa. Pia serikali ngazi ya Mkoa na wilaya inahusika na usimamizi wa ulinzi, usalama na utawala.
- Serikali za mtaa chini ya Halmashauri za Miji na Wilaya zina jukumu la kusimamia shughuli za uzalishaji mali, huduma za kiuchumi na kijamii, katika maeneo yao. Aidha utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri za Miji na Wilaya utazingatia sheria, kanuni na miundo yake.

Sekretarieti ya Mkoa ina wajibu wa kumshauri na kumsaidia Mkuu wa Mkoa kutekeleza majukumu yake pamoja na kuziwezesha Halmashauri za Manispaa na Jiji (support services) kutekeleza wajibu wao.

**Ndugu wadau,**

Nimenukuu majukumu hayo ya mgawanyo wa kazi kati ya Serikali Kuu na mamlaka za Serikali za Mitaa ili mfahamu kazi zao. Nafahamu katika barua zenu za wito wa kikao mmelezwa kuwa mtapata fursa ya kuelezea shughuli zenu, changamoto mnazopata na kama mnahitaji ushirikiano wowote kutoka ngazi za serikali. Hivyo mtumie fursa hii kufahamiana na kubadilishana uzoefu. Aidha katika utoaji wa huduma mnaweza kukutana na changamoto ambazo zinahitaji kushirikiana kuzitatua kulingana na mwelekeo wa utendaji katika mamlaka husika.

Mkoa wa Dar es Salaam kama mnavyofahamu tunazo changamoto nyingi kama vile za msongamano wa magari, upungufu wa miundombinu ya Afya, Elimu, Maji, Barabara, mifereji ya maji machafu na maji ya mvua, wafanyabiashara ndogo ndogo kuzagaa ovyo n.k. Ninyi kama wadau mnao wajibu wa kutafakari kwa pamoja namna ya kukabiliana na changamoto hizo na kushauri ufumbuzi wake kupitia malengo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu (short, medium and long terms).

**Ndugu wadau,**

Napenda nimalize kwa kutoa shukrani za kipekee kwa Katibu Tawala wa Mkoa kwa kubuni njia hii ya kukutana watendaji pamoja na viongozi wa taasisi za umma na madhehebu ya dini. Naamini juhudi hizi ndiyo mwanzo mzuri utakaokuwa endelevu katika kukabiliana na changamoto tulizonazo ili kufanikisha utoaji huduma bora kwa jamii.

Nawatakia mkutano mwema na wenye mafanikio. Baada ya kusema hayo sasa natamka kuwa mkutano umefunguliwa rasmi.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**